

Barua Kutoka kwa Uongozi wa Shule Kwenda kwa Familia- Toleo la siku

Ndugu Wazazi na Familia,

Kujua mahali ulipo na unapoelekea ni ufungo muhimu wa ukuaji na maendeleo. Shule yetu mara kwa mara hutumia taarifa za elimu ili kuweza kujua ni jinsi gani wanafunzi wanaendelea na kupanga mtaala wa ufundishaji ili kupata matokeo bora.

Hivi sasa serikali inatoa maelezo Zaidi kwa kutoa taarifa za mashule ya Iowa kwenye kadi ya Ripoti. Mfumo huu mpya wa taarifa mtandaoni utaweza kukupatia picha ya jinsi shule zote za serikali za Iowa nitavyofanya katika vipimo mbali mbali vya kielimu, kama vile, mahudhurio na viwango vya ufasaha wa wanafunzi.

Lengo la Kadi ya Ripoti ya mashule ya Iowa ni kutoa taarifa za elimu zitakazorahisishia wananchi kuzipata na kuelewa. Idara ya Elimu ya Iowa imetengeneza miundo mbinu kuambatana na sharia ya mwaka 2013(House file 215).

Shule hupewa alama kwenye Ripoti za Shule za Iowa kwenye vigezo vya elimu vipatavyo nane na alafu kupewa jumla ya alama kwenye vigezo vipimo vyote vya mashule. Muongozo ulioambatanishwa umetoa maelekezo ya vigezo vyote nane. Shule yetu imepata jumla ya alama **Kinakubalika!**

Wakati naamini ya kwamba maelezo haya yataboresha mjadala kuhusu maandalizi ya mafanikio ya wanafunzi, vipimo hivi ni kwa mujibu wa taarifa za mithani mmoja. Katika Jumuiya ya Mashule ya Cedar Rapids huwa tunatumia matokeo ya mitihani zaidi ya mmoja kila mara. Kama ambavyo tunafuata uadilifu kama kwenye Sheria ya No Child Left Behind, Shule ni zaidi ya lebo. Kwani lebo na alama hazielezei kila kitu.

Wakati nawahimiza kupambanua taarifa zilizotolewa kwenye Kadi ya Ripoti ya Iowa, vile vile ningependa uchukue muda kuijua shule ya mtoto wako. Tafadhali jisikia huru kuuliza maswali yeyote kuhusu mpango wetu wa kuboresha elimu na jinsi ambavyo unaweza kusaidia waalimu na wanafunzi wetu.

Unaweza ukapata matokeo katika tovuti yetu na vile viile taarifa Zaidi ya Kadi ya Ripoti ya Shule za Iowa katika tovuti ya Mashule www.cr.k12.ia.us. Madodoso ya taarifa Zaidi za Ripoti yamewekwa ili kukuwezesha kuelewa Zaidi. Vile vile unaweza kupata ripoti katika tovuti ya www.educateiowa.gov/schoolreportcard

Asante kwa ushirikiano wako na shule yetu.

Wako kwa dhiti

Mwalimu Mkuu